**Jarida la KVTC – 2025 Makala ya 2**

Tunafarijika kukaribisha kwenye Makala yetu ya mwisho 2025 ya jarida la KVTC. Mwaka huu tumeweka kumbukumbu nzuri tukiwa tunaimarisha shughuli zetu, tukizidisha mahusiano na jamii na kuimarisha majukumu yetu katika usimamizi endelevu wa misitu. Tunatarajia kuwa na mwaka mzuri kwa ukuaji, ushirikiano na mafanikio shirikishi.

Furahia kusoma!

**Mfanyakazi Mpya katika Familia ya Kampuni**



Bi Julie Ernest alijiunga na KVTC August 1, 2025 kama Meneja Raslimali watu na utawala anayesimamia kazi za raslimali watu, utawala, mahusiano ya wafanyakazi, utii wa sheria, uajili na uendelezo wa taasisi. Analeta uzoefu wa zaidi ya miaka 11 raslimali watu na uzoefu wa kisheria kwenye kilimo, ujenzi, mawasiliano na asasi zisizo za kiserikali. Alisha fanya kazi katika majukumu katika taasisi mbalimbali "Tree for The Future (NGO)", Agricom Africa Ltd, Seed Co Tanzania, Advent Construction Ltd, Larsen & Toubro, na Pact International (NGO). Ni mhitimu wa digrii ya LLB chuo kikuu Mzumbe na anasomea PGD KATIKA sheria za makampuni. Anaendelea kutoa mchango mkubwa KVTC.

**Angaza za Majukumu ya Kijamii:**



**Shindano la Wazo la biashara lisilo za Lisha taka**



Shindano la 2025 lili hamasisha wanafunzi kuandaa suluhisho la uzungushaji na endelevu katika dhima ya kutozalisha taka. Shule nane zilitoa mawazo ishirini. wazo lililoshinda ni kutoka Namwawala secondari na Greyson Gelvas Mtemele aliyependekeza kuzalisha mkaa wa kisasa kwa kutumia taka za karatasi, maji, udongo wa mfinyazi na vumbi la mkaa. Huu ubunifu unapunguza uchafu, unaleta mkaa safi, inapunguza mahitaji wa kukata miti, inasaidia kipato kwa vijana na inashabiana na malengo ya ya kampuni ya uhifadhi mazingira hususani inapo

fuatilia maswala ya ukiukaji ya uchomaji mkaa ambayo yalikuwa 29% ya matukio ya ukiukaji 2024.



**Shughuli za Kimichezo Kujenga afya na ushirikiano**

KVTC imeanzisha siku ya mwezi ya michezo lengo la kukuza afya, ushirikiano na maingiliano na jamii. Tukio la kwanza ni Octoba 2025 dhidi ya timu ya Msewa Academy Juniors. Timu ya mpira ya KVTC ina wanachama 41 ikiwemo wachezaji na washabiki. Mwenyekiti ni Conax Chisasa; Katibu – Angelous Lunyungu Kaptein – Msewa David. KVTC itatoa jezi uniform, mipira, viatu, filimbi, kisanduku za huduma ya kwanza bibs na kadi za referee.

**Maendeleo ya Kitengo cha Misitu Ukarabati wa Makazi**

KVTC inaendelea kuboresha makazi ya wafanyakazi kuboresha patikanaji

wa umeme, na kuimarisha upatikanaji wa maji katika makazi kwa mkakati wa mda mrefu. Mafinji shamba D uboreshaji umejumuisha maboresho ya jengo, umbile la ndani, paa jipya, sakafu, kupaka rangi na usafi. Umeme umeunganishwa na TANESCO na umeme wa jua.

**Ziara ya Wajumbe wa Bodi – Novemba 2025**



Wajumbe wa Bodi walitembelea KVTC Novemba 24 – 25, 2025 kwa kuona shughuli na



kutathmini mkakati. Matukio muhimu likiwemo ukaguzi wa bustani, maendeleo ya mradi wa majaribio ya mkaa, shughuli za mashambani na kutembelea mnara wa Humburu, Makazi ya Nakafulu na jitahada za ufugaji nyuki kwenye kikundi cha Wanjuchi na Kina mama  Itete.

**Matukio ya Afya za Wafanyakazi**



KVTC inaendelea kuimarisha program za afya na usalama kazini. Kampuni ina Kliniki yake inayosimamiwa na Afisa Uguzi Rogers Abisai na nessi Modesta Mpagama. Kliniki hii inatoa huduma ya kwanza kwa wafanyakazi wote walioko kwenye mashamba yake na kiwanda cha Mavimba.

Washiriki wa Mafunzo ya Huduma ya Kwanza



Kampuni inatoa mafunzo ya huduma ya kwanza kwa wafanyakazi wake na wale wa wakandarasi.

Kampuni imeshirikiana na Hospitali ya St Francis kusaidia kupima wafanyakazi dhidi ya magonjwa ya mfumo wa maisha na ushauri wa afya ya ubongo.

Kampuni inafanya jitihada kuhakikisha wafanyakazi wanapata vipimo vya HIV na kansa katika upimaji wa hiari na kuwasaidia katika matibabu kwa wale watakao kutwa na maambukizi au ugonjwa.